

KISWAHILI KWA KUFUNDISHIA: SERA NA MIKAKATI

Z. S. M. Mochiwa

Ikisiri

Makala haya yanajadili matatizo ya lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na vyuo. Makala yanaeleza kuwa matatizo wanayopata wanafunzi yanatokana na ukosefu wa msingi imara wa sarurufu ya lugha ya Kiingereza, ambayo hutumiwa kufundishia. Hali hii inawafanya wanafunzi kukosa stadi za kufikiri, kutambua na kuchambua mambo wanayojifunza kwa uhakika. Aidha, makala yanasisitiza kuwa kuna haja ya kubadili sera ya elimu ili kunusuru hali hii.

Pia, makala yanaeleza mambo muhimu katika utekelezaji wa sera mpya ya elimu. Baadhi ya mambo hayo ni: tamko rasmi la kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia sekondari na vyuo, uimarishaji wa ufundishaji wa lugha ya Kiingereza, uandaaji wa mitaala na uandaaji wa semina mbalimbali zitakazotoa msingi kwa walimu wa lugha ya Kiswahili.

Makala yanahitimisha kwa kueleza kuwa, utekelezaji wa sera mpya una mambo yafuatayo ambayo ni muhimu; tamko la sera, ushiriki wa wanajamii katika kutumia lugha, vyombo vya ukuzaji lugha pamoja na wataalam wa lugha.

1.0 Utangulizi

Tangu kuanzishwa kwa shule za mitaala ya kigeni nchini mwetu, matumizi ya lugha ya kufundishia yalikuwa yanalingana na makusudi ya elimu yenyewe. Kwa sehemu kubwa, makusudi ya elimu ya kikoloni na/au ya kimisheni yalikuwa kujenga stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Kwa mujibu wa Nyerere (1967), mfumo wa elimu katika enzi za ukoloni, haukukusudiwa kurithisha wapokeaji maarifa ya jadi na uzoevu wa jamii katika kuyamudu mazingira yao. Mfumo huo, badala yake, ulikusudiwa kuvunja jadi na uzoevu huo na kujenga maarifa na taratibu za kwao. (uk. 3).

Nyerere anaungwa mkono na Maxwell (1983) anayesema: Wamisionari waliamini kuwa elimu ni chombo madhubuti cha kuwatekea Waafrika wakaacha mila zao na kuukumbatia ukristo. (uk.xviii). Kwa msingi huu, shule zilikuwa na malengo mawili makuu. Kwa upande mmoja, zilitazamiwa zito watekelezaji wa mambo ambayo yanapangwa na watu wengine. Wahitimu wa shule hizo hawakutazamiwa kuwa chimbuko la fikra mpya. Wahitimu walikuwa na stadi hai za kukumbuka na kuiga. Aidha stadi hai za kuiga zilitimiza lengo la pili la elimu hiyo. Katika lengo hilo la pili, wapokeaji walitazamiwa kuwa na mwenendo mpya. Elimu ilikuwa chombo cha kuwajenga Waafrika wapokee imani mpya na kutupilia mbali mambo yote ya kizamani. Kwa ufupi, malengo ya elimu yalikuwa kuwatoa Waafrika vijijini mwao waende Ulaya.

Tanzania ilipopata uhuru, Nyerere (mtaje) alifanya tathmini ya kina ya elimu nchini na kuipatia makusudi mapya. Dhima ya elimu, kwa mujibu wake, ni kumwezesha mpokeaji ajitambue na ajijengee stadi za akili na mwili za kumfanya ajitegemee, atanzue tata na awe na fikra angavu. Mhitimu wa elimu hii awe mweledi wa vipawa vyake na pia awe na uwezo wa

kujiamini. Elimu hiyo impe ujasiri wa kuwa mtangulizi badala ya kuwa mlungizi. Msisitizo wa elimu hii uwe katika kumpa changamoto mpokeaji kiakili na kimwili ili amudu kujisawiri na kuyasawiri mazingira yake. Mtalaa unaokidhi malengo ya elimu ya namna hii uwe ule unaoibukia ndani ya utamaduni wa mpokeaji, na ambao, unazingatia mahitaji yake katika viwango vyote vya makuzi.

Kasoro kubwa iliyojitokeza, na tukabaki nayo hadi leo, ni kwamba falsafa iliyomo katika elimu ya kujitegemea haikutoa msimamo kuhusu matumizi ya lugha madarasani. Badiliko lililotokea baada ya kutangazwa kwa falsafa hiyo ni matumizi ya Kiswahili kwa kufundishia elimu ya msingi tu. Badiliko hilo lilileta athari maradufu. Mosi, limeifanya elimu ya msingi ‘kupungua thamani’ machoni mwa Watanzania. Elimu hiyo ilionekana kuwa ya ‘kienyeji’ kwa kuwa inafundishwa kwa lugha ya ‘kienyeji’; Kiswahili. Ni elimu ya kila Mtanzania aliye, na, asiye na akili.

Tunapoichunguza tathimini hii kwa makini, tunaona kuwa hisia za Watanzania ni kuwa elimu ya kweli kweli haifanuki kwa lugha ya kienyeji. Aidha, moja ya sababu zilizoifanya Tanzania isibadili lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na vyuo vya juu hadi leo, ni kwa kuwa Kiswahili hakionekani kuwa kinaweza kufafanua mambo makubwa ya kisayansi. Madai haya ni zao halisi la historia yetu ya kutawaliwa pamoja na matokeo ya elimu iliyowataka wapokeaji kuukana Uafrika wao. Isitoshe, elimu inayotolewa shuleni imebakia kuwa ya Wazungu na Uzungu; si elimu ya kumwezesha mpokeaji kuyamudu mazingira yake.

Watu wengi waliopata kutawaliwa, na hasa waliopata elimu ya kikoloni huelekea kudharau vya kwao na kutukuza vya aliyekuwa mtawala wao. Mulokozi (2000) anasema hata vitambulisho vyao kama vile lugha au utamaduni kwa ujumla ni wa aliyekuwa mtawala wao. Kwa kusema hivyo, Mulokozi anajibu swali la Tollefson (1991) lililotafuta sababu ya Kiingereza kuwa lugha ya Namibia huru, hata kama inazungumzwa kizawa na weupe wachache tu. Kwa kuwa malengo ya elimu ni kuuboea Uzungu, elimu isiyofundishwa kwa Kizungu hupoteza thamani yake.

Athari ya pili ya badiliko la lugha ya kufundishia elimu ya msingi tu ni kukatika kwa mfululizo wa usawiri wa mpokeaji. Matumizi ya lugha mbili za kufundishia: Kiswahili katika shule ya msingi na Kiingereza katika sekondari na vyuo vya juu, yanasababisha mgawanyiko wa mtalaa kiakili au kisaikolojia. Mwanafunzi aliyemaliza shule ya msingi akabahatika kuliona darasa la kidato cha kwanza hujigundua kuwa mbumbumbu kutokana na kushindwa kuelewa Kiingereza. Dhana alizozioea hazisawiriki kwake kwa kuwa zimemezwa na lugha mpya ya kufundishia. Hivyo ni kusema, kuingia kidato cha kwanza si kuendeleza uzoovu uliopatikana katika elimu ya msingi, bali ni kuanza mtalaa mpya na kusahau wa zamani. Hali hii imemfanya Mochiwa (1999:46) adai kuwa uzoovu wa mwanzo haumsaidii bali huwa kikwazo. Hali hii inazidi kutuonesha kuwa malengo ya elimu tuliyorithi enzi za ukoloni hayajabadilika. Mfumo wa elimu, kama ilivyokwisha semwa nyuma, humfanya mpokeaji asahau ya kale akumbatie mapya. Elimu inayotolewa kwa mtindo huu, huwafanya wahitimu wake kuwa wepesi wa ‘kwenda na wakati’. Wao wanathamini leo yao tu, lakini hawana nafasi ya kufikiria jana yao wala kesho yao.

Katika umri wake wote, Jamhuri ya Tanzania iliendelea kufumbia macho kasoro hii kwa kukosa ujasiri wa kuikabili uso na macho. Badala yake, Jamhuri ikaendelea kuliundia tume suala la lugha ya kufundishia. Jamhuri, kwa mfano, iliunda Tume ya Makwetta (1982) ambayo ilipendekeza Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia. Baada ya kulikataa pendekezo

hilo, ndipo wakachukua hatua nyingine ya kuchelewesha (au tuseme kuzuia?) mabadiliko yatakayoinusuru elimu nchini. Katika hatua hiyo, Jamhuri ilitoa agizo kwa vyombo vya ukuzaji wa Kiswahili, kuiandaa lugha hiyo kwa ajili ya mabadiliko yanayofikiriwa. Wakati huohuo, wazazi na wananchi, kwa ujumla, walialikwa wajaadili kufaa na/au kutofaa kwa badiliko la lugha ya kufundishia. Mwenendo huu wa Jamhuri ni ushahidi imara wa dai alilotoa Heugh (1999) aliposema:

Historia ya mahusiano kati ya lugha na elimu barani Afrika, katika karne hii, ni ile ya kuendelea kuunda tume moja baada ya nyingine na tume zote hizo huibuka na hitimisho moja la matumizi ya lugha asilia katika elimu..

Viongozi wa nchi hii hawana budi kujiuliza maswali kuhusu uelewa wao wa suala hili la lugha ya kufundishia. Miongoni mwa maswali ya kujiuliza ni haya: Ni kwa kiasi gani wale waliopata kulichangia wanajua nafsi ya suala lenyewe? Je, wanajua kinachowalemea wanafunzi ndani ya Kiingereza cha kufundishia? Wanaohoji uwezo wa Kiswahili wa kukidhia haja ya elimu ya juu wanajua lugha ni nini? Laiti wangejua, wangethubutu kuuliza swali kuhusu uwezo wa Kiswahili? Aidha, maelekezo ya kuandaa Kiswahili kwa majukumu mapya yanatokana na ujuzi wa nafsi ya lugha? Ni kwa vipi lugha ya Kiswahili ikuzwe na kikundi cha watu nje ya matumizi? Maelekezo haya hayafanyi lugha katika jamii kuwa gwanda ambalo, mara baada ya kushonwa na fundi maalumu, linamtosha kila mwanajamii? Hizi ni miongoni mwa fikra ambazo tumedumu nazo hadi sasa.

Aidha, mwelekeo wa kutafuta mjadala na mwafaka kwa wananchi kuhusu badiliko la lugha hutuhumika kwa namna mbili. Kwa upande mmoja, ni vigumu kwa mtu kukwepa tashiwishi kuwa Jamhuri haina nia safi ya kuleta badiliko hilo. Kwa hivyo, kualika wananchi katika mjadala wa lugha gani itafaa kufundishia ni mbinu ya kulizuia au kulichelewesha. Kwa upande wa pili, ni rahisi kuamini kuwa, Jamhuri haielewi kwa undani nafsi ya tatizo wala nafsi ya ufumbuzi wake. Jamhuri ilitarajiwa kujua kwamba, katika suala zito kama hili la kitaalam, wazazi au Watanzania wa kawaida wasingeweza kutoa mchango wowote isipokuwa wa kihisia tu. Lakini badiliko la lugha si suala la kuamuliwa kihisia. Wazazi wa Tanzania si tofauti na wale waliolaumiwa na Taylor (1981) aliposema:

Wazazi wa Afro-Caribbean wana wahka kuhusu watoto wao lakini hawaelekei kuelewa umuhimu wa michezo, mawasiliano na makusano kati yao na watoto wao.

Wazazi wa Tanzania, kama wale wa Afro-Caribbean, wana wahka kuhusu watoto wao lakini hawaelewi undani wa tatizo la watoto wao. Hawana uwezo wa kulisawiri tatizo hilo. Wazazi hawa hawana makusano na watoto wao kwa kuwa lugha wanayojua na kuendeshea maisha nyumbani mwao ni tofauti na ile ambayo watoto wao wanatumia shuleni kwao.

Makala haya yana makusudi matatu: kwanza yanatoa pendekezo la sera ambayo itaunusuru mfumo wa elimu. Katika pendekezo hilo, jambo muhimu si kung'oa lugha moja na kupandikiza nyingine. Makusudi ya sera hiyo ni kuleta mpangilio mpya wa dhima za lugha mbili za makuzi nchini; Kiswahili na Kiingereza. Pili, makala yanakusudia kuonesha hatua kwa hatua utekelezaji wa sera hiyo mpya. Katika hii hiyo, makala yataelekeza nafasi ya serikali, asasi za ukuzaji wa Kiswahili nchini pamoja na nafasi za wataalam wa fani mbalimbali. Hali kadhalika, makala yatajadili maandalizi muhimu yatakayoandamana na utekelezaji wa sera hiyo. Kabla ya kuingia katika pendekezo lenyewe, inabidi makala yafafanue suala la msingi.

2.0 Suala la Msingi

Suala la msingi limo katika vipengele vitatu. Kwanza, hapana budi kile kinachowashinda wanafunzi shuleni kifahamike vyema. Tunaposema kuwa wanafunzi hawawezi Kiingereza, tuna maana kuwa, wanashindwa kumiliki sarufi ya lugha hiyo. Wanashindwa kusuka na kusukua tungo za Kiingereza kutokana na kutokuwa na ujuzi thabiti wa sarufi ya Kiingereza. Mweka wa kauli hii ni kwamba, nafsi ya lugha yoyote ni sarufi yake. Sarufi ndiyo inayochukua upekee wake. Hivyo basi, sababu ya pendekezo la badiliko la sera ni kwamba, kwa kushindwa kuimiliki sarufi ya Kiingereza ina maana kuwa wanafunzi hawajui lugha hiyo.

Tunapokubaliana kuwa nafsi ya lugha ni sarufi, madai ya kusema, Kiswahili hakiwezi kufundishia elimu ya sekondari hayana msingi wa kisayansi. Madai haya ni sawa na kusema Kiswahili hakina sarufi au kina sarufi changa. Watu wengi wanaopinga badiliko la sera wanatuingiza katika kipengee cha pili cha mkanganyiko kuhusu suala la msingi. Wako watu wanaokataa Kiswahili kufundishia elimu ya sekondari kwa sababu hakina msamiati. Kwa watu wa aina hii, lugha ni msamiati. Lakini tatizo la upungufu wa msamiati – na ni lazima sote tukiri kuwa lipo – linaweza kupungua uzito endapo sote tutaifasili nafsi ya lugha kwa kutumia sarufi yake. Kitaalam, kila lugha ina sarufi yake kamili.

Aidha, tunapoifasili lugha kisarufi haiwezi kuwa vigumu kuona kuwa msamiati wa Kiswahili utakua kwa kulingana na jinsi kinavyotumika. Vilevile, vipengele vya msamiati ambavyo vinakosekana sasa, huweza kuchukuliwa kutoka kwenye lugha nyingine yoyote. Hivyo, kama ilivyokuwa kwa lugha ya Kiingereza, Kiswahili kitavuna msamiati ndani ya matumizi yake. Laiti nafsi ya lugha ingalikuwa ni msamiati, Kiingereza kisingalipata sifa ya kuwa lugha kubwa duniani kwa sababu ina asilimia ndogo ya msamiati wa asili. Sehemu kubwa ya msamiati wake ni wa mkopo.

Jambo jingine litakalochimbuka mara tutakapoifasili nafsi ya lugha kuwa sarufi yake ni kwamba tutaondokana na rai isiyo ya kisayansi ya kuandaa lugha kwa ajili ya majukumu ya baadaye. Haitakuwa vigumu kuelewa kuwa lugha yoyote hunyumbukia matumizi yake mapya. Hivi leo, Kiswahili kikawa na vipengele vya msamiati kama vile *mstatili*, *mraba*, *pembenyofu*, *giligili*, *fuwele*, *akisi*, n.k., ni matokeo ya matumizi yake katika shule za msingi.

Hali kadhalika, kinapokuwa kihalisi chetu sote kuwa lugha ni sarufi yake, tutakuwa tumesogelea kipengee cha tatu: dhati ya tatizo la wanafunzi shuleni. Itakuwa rahisi kwetu kuelewa kwa nini wanafunzi katika madarasa ya sekondari hawawezi kushiriki katika makusano na walimu wao. Itakuwa vyepesi pia kuelewa sababu za wahitimu wa elimu ya sekondari na vyo vya juu kukosa stadi za kufikiri, kutambua na kuchambua mambo kwa akili zenye uhakiki. Kukosa uwezo wa kuimudu sarufi ya lugha ya kufundishia ndilo chimbuko la kukosekana kwa wahitimu wenye akili zinazochata. Badala yake, wahitimu wanaambulia akili zinazonata zenye uwezo wa kukariri mambo tu (taz. Mochiwa 2000).

Kutokana na kutoelewa nafsi ya tatizo hili la elimu pamoja na badiliko linalopendekezwa, baadhi ya wanaounga mkono kuendelea kwa Kiingereza kwa kufundishia wanaelewa kuwa pendekezo la badiliko ni la kuling'oa Kiingereza hapa nchini. Watu hao wanafikiri kuwa Kiswahili kinapoingia sekondari, Kiingereza hakitakuwa na nafasi kabisa. Kutokuelewa huko

kumelifanya badiliko linalokusudiwa kuleta kitisho kwa kila mtu anayejua nafasi ya Kiingereza katika zama hizi. Kwa kuelewa kuwa Kiingereza ‘kitapigwa marufuku’ nchini, watu wengi wamejiuliza: Kiswahili kina vitabu vya rejea? Kwa kuwa jibu la swali hili si ‘ndiyo’, ndipo wakapendekeza vifasiriwe vitabu vya kiada na vya ziada kabla ya kuanza kwa utekelezaji. Kwa ufupi, wataalam wanapendekeza ijengwe maktaba ya Kiswahili kwanza kabla ya kuliingiza badiliko hilo la lugha ya kufundishia.

Badiliko linalopendekezwa halikusudiwi kung’oa Kiingereza. Endapo litaangaliwa kisayansi, badiliko la sera litaimarisha Kiingereza nchini. Tena, badiliko hilo litainua viwango vya ujuzi wa kuzitumia lugha zote na kwa manufaa zaidi. Kwa kuwa pendekezo hili ni la sera ya lugha mbili katika elimu, Kiswahili na Kiingereza, kuing’oa hii lugha ya pili kwa sababu yoyote ile, ni kulifanya pendekezo lisitekelezake. Kwa mujibu wa sera hiyo mpya, kila lugha itapangiwa dhima zake mahsusi, kama itakavyodhihirika hivi punde. Katika sehemu inayofuata, tunafafanua lugha zinazoendesha maisha ya Watanzania.

3.0 Matumizi ya Lugha Zilizopo

Mtaalam mmoja, Pool (1972), alipata kusema kuwa wingi wa lugha katika nchi changa ni miongoni mwa dalili za uchanga wa nchi hizo kimaendeleo. Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo ambazo zina lugha nyingi. Wengi huu wa lugha unaleta umaskini mkubwa wa kimawasiliano. Watanzania walio wengi wana lugha za makabila yao. Lugha hizi ndizo zinazowapa pumzi yao ya kwanza ya kijamii. Kwa kuzijua lugha hizi, Watanzania husharabu adabu za kwao, taratibu za makusano katika jamii zao. Kwa kutokana na lugha hizi, Watanzania hupata kujua mahusiano yao na wale wanaowazunguka. Kwa ufupi, lugha hizi ndizo za malezi yao (Taz. Mochiwa 1999). Lugha hizi za kikabila zinakisiwa kuwa zaidi ya mia moja na ishirini.

Katika mfumo wa elimu nchini Tanzania, Kiswahili hufundishia shule za msingi. Wanapojiunga na shule hizo, wanafunzi wanalazimishwa kuacha lugha za malezi ambazo ndizo wanazozijua. Kutokana na lazima ya shule, wanafunzi hao hujifunza Kiswahili hadi ya kukimiliki (ang. Mochiwa 1999). Kwa kuwa lugha za malezi zilizo nyingi ni za Kibantu, changamoto ya kubadili lugha hubebeka bila ya maumivu na bila ya uwezekano wa mwanafunzi kushindwa. Aidha, Kiswahili kinafundishika, kwa sababu, zaidi ya kuwa lugha ya Kibantu, kinasikika katika mazingira yao kwa mapana na marefu. Kiswahili ndicho kinachoendesha maisha ya Jamhuri.

Wanapoingia katika shule za sekondari, wanafunzi walewale hubadilishiwa tena lugha watakayofundishiwa. Safari hii, wanafunzi hao hulazimishwa watumie Kiingereza. Kwa ufupi, watoto wa Tanzania hulazimishwa waache Kiswahili, lugha wanayojua vizuri, na kupokea maarifa kwa Kiingereza, lugha wasiyojua. Sasa, ingawa mabadiliko haya ya lugha yanaonwa na kila mtu, lakini kuna wasiwasi kuwa hayaeleweki kwa jinsi ileile na/au uzito uleule. Wasiwasi wetu huu unatokana na aina ya vikwazo vinavyotolewa na wale wasiokubaliana na badiliko linalopendekezwa.

Kimsingi mfumo wa elimu hutumia lugha mbili: Kiswahili na Kiingereza. Kiswahili hutumika kwa kufundishia elimu ya msingi, na Kiingereza kwa ajili ya elimu ya sekondari. Hizi ndizo ambazo zinasuhulisha mawasiliano na makusano kati ya wanafunzi na walimu wao. Ikisemwa vinginevyo, lugha mbili hizi ndizo zinazowawezesha wanafunzi waulize,

waeleze, wahoji rai zinazotolewa, wazikatae au waziunge mkono. Kwa kutumia lugha hizi, wanafunzi wanatazamiwa washikilie au waachilie rai zao au wazirekebishe kwa kulingana na mijadala itakayokuwa inajisokota ndani ya makusano yao. Lugha hizi zinatazamiwa ziwape uwezo wa kusasanya na kusasanyua mambo. Ni dhahiri kuwa, kuingiza Kiswahili katika shule za msingi na baadaye Kiingereza katika shule za sekondari kunaleta madhara ya kitaaluma na kisaikolojia pia.

Kwa maana hiyo, mtoto anapoingia shule ya msingi hunyang'anywa lugha ya kikabila aliyozoea na kulazimishwa kutumia Kiswahili ambacho kwa wakati huo hakijui vizuri. Hili ni badiliko ambalo, kama nilivyopata kusema kwingineko (Taz. Mochiwa Mtaje), hutenganisha uzoovu uliopatikana wakati wa malezi na ule utakaopatikana katika makuzi ya kwanza, ya shule ya msingi. Aidha kutokana na badiliko la lugha, dhana mbalimbali zilizopatikana kwenye lugha hiyo ya malezi huweza kupotea au kuparaganyika (Mochiwa Mtaje).

Kwa bahati nasibu tu, Kiswahili, lugha ya kwanza ya makuzi, kina nasaba kubwa na lugha nyingi za makabila. Ubuntu wake unakifanya Kiswahili kiwe na msamiati na sarufi ambayo hukaribiana sana na lugha hizo. Inasemekana kuwa zaidi ya asilimia hamsini ya msamiati wa Kiswahili una asili ya Kibantu (Taz. Guthree). Kweli hii ya kihistoria imekuwa chimbuko la wepesi kwa watu wanaozungumza lugha yoyote ya Kibantu kukidaka na kukisharabu Kiswahili.

Badiliko la kumlazimisha mwanafunzi kuacha lugha ya kikabila na kutumia Kiswahili halileti misukosuko mingi ya kisaikolojia. Mara nyingi, baada ya mwaka au miaka miwili mwanafunzi hukimiliki Kiswahili kwa kiwango cha kumwezesha kukitumia kwa kuchanuzia masihara au kweli ya uzoovu wake. Hivyo, katika kipindi kifupi, Kiswahili humwia mwanafunzi chombo thabiti cha kupokelea na cha kuchanuzia maarifa, taarifa na hisia zake. Ikisemwa vinginevyo, mwanafunzi hupata uwezo wa kusuka semi zake na wa kusukua, yaani kuelewa kikamilifu, semi za wenzake, zikiwa ni pamoja na za walimu wake.

Baada ya kujenga msingi thabiti wa ufahamu wake wa Kiswahili, mwanafunzi huyo hunyang'anywa Kiswahili na kukabidhiwa Kiingereza kuwa lugha yake ya kujifunzia. Badiliko hili linamjia baada ya kuwa amejifunza Kiingereza katika shule ya msingi kwa jumla ya saa zisizozidi mia nane (800) (Mochiwa 1991). Wataalam na/au viongozi wa Tanzania wameridhika kabisa kuwa baada ya kufundishwa Kiingereza na walimu hawa waliopo hapa nchini kuanzia darasa la tatu hadi la saba, kwa idadi hiyo ya saa na kwa vifaa hivi tulivyo navyo, Kiingereza kitakuwa kimefundishika na kitakuwa chombo cha kusukia na kusukulia maarifa ya shule za sekondari.

Kwamba mwega wa sera ya aina hii ni muujiza wa Mwenyezi Mungu, huthibitika kwa njia mbili. Mosi, kwa utafiti uliopo, haiwezekani kuisharabu lugha ya malezi bila ya kutumia saa 18,000 (Hammerly 1982). Hii ina maana kuwa, kabla ya kuingia shule, mwanafunzi alitumia miaka mitano au sita ya kwanza ya maisha yake kwa kujifunza lugha ya malezi. Muda huo ndio uliomwezesha kujenga msingi thabiti wa sarufi ya lugha hiyo. Aidha, katika kujenga msingi huo, mtoto alisaidiwa sana na mazingira yake. Watu wote waliokuwa wamemzunguka walikuwa wakizungumza lugha anayojifunza. Isitoshe, katika kipindi hicho, mtoto hakuwa na shughuli nyingi alizopangiwa ambazo zilihitaji makini ya akili yake. Kwa ufupi, mtoto hakuwa na ratiba nyingine rasmi ya kumshughulisha kiakili. Ni dhahiri kuwa, kumtazamia mtoto ajifunze Kiingereza darasani kwa muda mfupi kama huu, ni kutarajia muujiza.

Pili, usharabu wa Kiingereza, ambayo ndiyo lugha ya makuzi katika kiwango cha sekondari, hutegemea kufundishana tu. Hii ina maana kuwa usharabu unatokana na mtoto kuwa mwanafunzi wa mwalimu fulani. Ubaya wa utaratibu huu wa usharabu ni ule uwezekano wa kuathiriwa na kiwango duni cha mwalimu, zana duni za ufundishaji na ukosefu wa mchango wa mazingira katika kuimarisha stadi zinazofundishwa.

Aidha, inapokumbukwa kuwa, kinapofundishwa, Kiingereza hakina matumizi ya papo kwa papo, ndani wala nje ya darasa, jitihadi zote za kukisharabu ni kama mchezo wa kuigiza. Mwanafunzi anapata jina la *'Betty'* na mwalimu *'Mr. Winterbottom'*. Kwa maneno mengine, msemu wanaojifunza hauhitajiki kuendeshea maisha yao sasa hivi! Hapana shaka kuwa, usharabu huu haupati msukumo ambao, kila mwanadamu anao (Klein 1986) wa kujifunza lugha ili kujitafutia nusura. Mtoto aliitafuta lugha ya malezi ili aunganike na familia yake. Kutokana na nasaba yake na lugha ya kikabila, Kiswahili kilikuwa chepesi kwa mtoto. Hivyo sivyo ilivyo kwa Kiingereza.

Ama, wanaoshikilia kuwa inawezekana kuisharabu lugha ya Kiingereza wanaegamia katika mwafaka kuwa kila Mtanzania ana kipawa cha kujifunza lugha. Hatuhitaji kufanya utafiti kugundua kuwa wepesi wa kusharabu lugha ni kipawa kimoja miongoni mwa vingi ambavyo watoto huzaliwa navyo. Vipawa vingine ni kama wepesi wa ufahamu wa hisabati, jiografia, historia, kemia, fizikia, n.k. Tunapokubali kuwa usharabu wa lugha hutegemea kipawa cha mwanafunzi na mwalimu wake, hatuwezi kutafuta muujiza uwamiminie wanafunzi lugha ya Kiingereza kwa muda wa saa mia nane.

Pamoja na ugumu wa usharabu unaowakabili, wanafunzi hulazimika, baada ya kuvuka kiwango cha elimu ya msingi, kutumia Kiingereza kupokelea changamoto za elimu ya sekondari na vyuo vya juu. Wanatazamiwa hivyo hivyo kimiujiza miujiza, wasuke fikra zao na hapohapo wamudu kusukua fikra za walimu na za wenzao zilizosukwa kwa lugha hiyo ya Kiingereza. Wanafunzi hao wanatazamiwa wajenge ari ya kusoma vitabu vya Kiingereza na wanaposoma waelewe na papo hapo waweze kutambua, kuchambua, kusasanya na kusasanyua yale waliyosoma. Kwa maana nyingine, Kiingereza kina dhima ya kukuza dhigni za wanafunzi ili mwisho wa mchakato wao wa elimu waweze kuwa chimbuko la fikra angavu. Wahitimu hao wanatazamiwa kuwa na akili zinazochata badala ya zile zinazonata.

Kutokana na hima kubwa ya serikali kuhakikisha kuwa Kiingereza kimo ndani ya maisha yetu kwa mtindo huu, Kiswahili kikaendelea kudumaa, kikabaki lugha ya kuuzia nyanya. Kiswahili kinaendelea kuwa lugha ya mambo yasiyo ya kitaalamu. Mtu, kwa imani iliyopo nchini, hawezi kuwa mtaalam ikiwa harogonyi lugha isiyojulikana katika mazingira yake. Lakini pamoja na ufili – ubishi usio na hoja – ninadhani ndani ya jamii hii wengi wanajua kuwa muujiza unaotazamiwa hauwezi kuwa.

Pengine hii inatupatia fununu ya sababu ya nchi yetu kusita kuwaamini wahitimu wetu, kwani wanajua fika kuwa, wamepata matatizo katika mchakato wao wa elimu. Aidha, hakika ya tatizo la mchakato wetu wa elimu kuzaa akili zinazonata tu, linaonekana kuwa matokeo ya mbinu za nchi za Magharibi za kuhakikisha kuwa mifumo ya elimu ya nchi changa inaendelea kutoa wahitimu wasio na uwezo wa kufikiri. Mazrui (1997) anasema kuwa uongozi wa nchi changa haung'ang'anii – Kiingereza kwa hiari yao. Nchi za Magharibi hutumia matumizi ya Kiingereza kudhoofisha elimu ili nchi changa ziwe mlimbi mkubwa wa kupatia wafanyakazi walungizi si wafanyakazi, watangulizi.

Uamuzi wa kuleta badiliko la lugha ya kufundishia unatokana na umaizi wa mambo makuu matatu. Na ingawa yamejadiliwa, kuyataja kwake ni kujiweka tayari kwa badiliko lenyewe. Jambo la kwanza lililojadiliwa ni kule kutokuelewa kwa usahihi tatizo la Watanzania ni nini katika elimu. La pili ni kutokuelewa lugha ni nini? Na la tatu ni kule kutofahamu kuwa zoezi la kusharabu lugha lina gharama kubwa ya wakati, mali na nguvu kazi. Kulielewa tatizo la elimu Tanzania, ni hatua muhimu katika kusawiri mbinu za utekelezaji wa sera mpya ya lugha ya elimu.

4.0 Badiliko la sera

Badiliko la sera inayopendekezwa lina hatua tatu kuu. Hatua ya kwanza inatekelezwa na serikali na hatua ya pili inatekelezwa na wataalam wa lugha. Hatua ya mwisho inatekelezwa na wataalam wote katika fani mbalimbali za elimu. Isitoshe, utekelezaji wa hatua mbili za mwisho ni zoezi la kudumu. Tuangalie yanayofanyika katika hatua ya kwanza.

4.1 Tamko la badiliko

Hatua ya kwanza katika kuleta badiliko hili ni tamko la serikali kuhusu dhima za lugha mbili zilizomo katika mfumo wa elimu. Katika tamko hili, Kiswahili hupewa dhima ya kukuzia akili na dhahiri za Watanzania. Kwa uamuzi huo, Kiswahili kinatamkwa kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na ile ya vyuo vya juu. Zaidi ya hayo, hapana budi ifafanuliwe wazi wazi kuwa Kiswahili kitaendesha mijadala yote ya kitaaluma ndani na nje ya madarasa. Hali kadhalika, tathmini zote za elimu katika viwango mbalimbali vya mfumo mzima wa elimu zitafanyika kwa Kiswahili.

Katika hatua hiyo ya kwanza, hapana budi serikali itoe ratibu ya utekelezaji wa badiliko linalokusudiwa. Muhimu hapa ni kutamka ni lini Kiswahili kitaingia katika madarasa ya sekondari. Vivyo hivyo, itabidi itamkwe wazi badiliko hilo litaanzia wapi. Ikiwa itasibu vyema kupendekeza, itakuwa vizuri kwenye tamko hilo kuwe na muda wa miaka kama mitano kati ya tamko na utekelezaji wake. Hii ina maana kuwa wanafunzi watakuwa waanzilishi wa badiliko la sera, wawe wameandaliwa kwa miaka mitano ya shule ya msingi kwa kutumia mitalaa mipya inayofundisha stadi za kusoma na kuelewa Kiingereza. Hapana shaka kuwa, kwa utaratibu huu, badiliko litaanzia kidato cha kwanza.

Utekelezaji wa sera ya Kiswahili kwa kufundishia ni hatua ya kwanza kabisa ya kujengea msingi madhubuti wa maendeleo ya kijamii. Makusudi ya kauli hii ni kwamba mara itakapotekelwa, sera hii mpya itawapatia Watanzania fursa sawa za kujikuza kiakili na kidhahiri kwa kulingana na vipawa vyao. Aidha, utekelezaji huo, utabadilisha maana ya shule na elimu kwa jumla. Kwa sasa, elimu ni mauzauza au mambo ambayo hayaeleweki na hayana mnasaba wa moja kwa moja na maisha. Elimu, kwa sasa ni giza giza linaloashiria ufahamu nusu nusu.

Kuingia kwa badiliko la Kiswahili kufundishia elimu ya juu kuleta arabuni ya kupatikana kwa akili zinazochata. Isitoshe, badiliko linapoiningia linaanzisha ukurasa mpya wa kuifanya elimu kuwa maisha badala ya kuwa mchezo wa kuigiza. Elimu itaelekea katika ujenzi wa stadi mbalimbali zitakazodhihirisha ukuaji wa akili pamoja na uwezo wa kufikiri. Hapana shaka kuwa, hata tathmini ya elimu hiyo itakuwa na lengo la kupima uwezo na viwango vya

utanzuaji tata badala ya kupima kumbukumbu ya mwanafunzi tu. Kutokana na badiliko hilo, shule itabadilika kuwa mahali ambapo mwanafunzi anasaidiwa agundue na kukuza vipawa vyake.

Katika tamko hili, hapana budi ielezwe wazi kuwa badiliko la sera linazingatia ukweli wa kiisimu kuwa nafsi ya lugha imo ndani ya sarufi yake. Msamiati wa lugha yoyote huweza kujipenyeza katika lugha yoyote na ukatumika. Kwa mantiki hii, Kiingereza kinaporithiwa na Kiswahili katika kufundishia, Kiingereza kitakiachia Kiswahili msamiati wake wote unaohitajika katika ufafanuzi na uchambuzi wa fikra za kitaalamu. Hili si jambo jipya na wala haliharibu nafsi ya Kiswahili. Aidha, Kiswahili hakitakuwa cha kwanza kusharabu msamiati wa kigeni ndani ya msamiati wake.

Uamuzi wa kukipangia Kiswahili majukumu mapya unakwenda sanjari na uamuzi wa kukipatia Kiingereza majukumu yake. Muhimu katika majukumu hayo ni lile la kukifanya kuwa lugha ya maktaba. Hii ina maana kuwa Kiingereza kitatumiwa na wanafunzi na walimu kwa ajili ya kusoma vitabu vya marejeo. Kwa mantiki hii, wanafunzi na walimu wao hawana budi wawe na uwezo wa kusoma na kuelewa matini zilizoandikwa kwa Kiingereza. Vitabu vyao vya kiada na ziada vitakuwa vya Kiingereza, tena pengine, kwa muda mrefu. Kwa sababu hiyo, utekelezaji wa matumizi ya Kiswahili kwa kufundishia hauna budi kwenda sambamba na uimarishaji wa stadi za Kiingereza za ufahamu wa kusoma Kiingereza. Ujuzi huu wa Kiingereza si wa muda bali ni wa kudumu kwa vile humpa uwezo mwalimu au mwanafunzi kuingia katika uwanja wa taaluma yake ambao umeandikiwa kwa lugha ya Kiingereza kwa miaka mingi.

Kukifanya Kiingereza kuwa lugha ya maktaba kunaondoa hofu iliyopo ya ukosefu wa vitabu vya kiada na ziada. Wakati wa utekelezaji wa sera, waalimu na wanafunzi wao watakuwa wameandaliwa kwa kuwa na stadi maalum za Kiingereza ambazo zitawawezesha kutumia maktaba zao ambazo zimejaa vitabu vya namna mbalimbali. Pengine itafaa kusisitiza hapa kuwa, ujenzi wa stadi hizi za Kiingereza zinazotakiwa si mgumu na pengine hata gharama yake ya wakati na mali si kubwa. Mpaka sasa, wanafunzi karibu wote hupata taabu kuelewa wanachosoma kwa Kiingereza lakini ugumu huo huongezeka maradufu wanapotakiwa kujieleza au kueleza yale wanayosoma kwa lugha hiyo. Stadi za kuelewa lugha ya kigeni huimarika mapema kuliko zile za kujieleza. Ni dhahiri kuwa, Uwezo wetu mdogo wa kiuchumi uliopo utatumika kwa busara zaidi kwa kuwapatia walio wengi stadi za ufahamu wa kusoma Kiingereza badala ya ule wa kusomea Kiingereza.

Baada ya kuondoa kundi kubwa la wanafunzi ambao, kwa jumla, hawana kipawa cha lugha, inapatikana nafasi ya mafunzo maalum ya Kiingereza. Mafunzo hayo yatawahusu wanafunzi wenye kipawa dhahiri cha lugha. Hawa ndio ambao watafundishwa kikamilifu ili wawe na stadi zote za Kiingereza. Wahitimu wa mafunzo haya watategemewa kuiunganisha Tanzania na nchi nyingine ulimwenguni. Wahitimu hawa, kutokana na kipawa chao cha lugha, ndio wanaoweza kuwa wakalimani na wafasiri. Kuimarisha mafunzo ya watu wenye kipawa cha lugha kutailinda nchi hii dhidi ya watu wa nje wasioitakia mema. Ujuzi nusu nusu wa Kiingereza unaweza kuifanya nchi iridhie mikataba ambayo, bila ya kuelewa, huhatarisha uhuru au uchumi wa nchi.

Ili utekelezaji ufanikiwe, hapana budi serikali ikane matumizi ya Kiingereza katika mawasiliano yake ndani na nje ya nchi. Nchi hii haiwezi kuheshimiwa ikiwa inaendelea kwa kufadhiliwa hata lugha. Uongozi mzima wa nchi utakapokumbatia Kiswahili, kutatokea

mabadiliko makubwa katika mabaraza ya kimataifa kama vile UNO, OAU, n.k. Kwanza, Kiswahili kitaingia katika mashirika haya ya kimataifa. Hii itakuwa hatua muhimu ya kukiuza Kiswahili nje ya nchi. Pili, ikiwa Jamhuri itakikumbatia Kiswahili kwa kukifanya kiendeshe shughuli zake za nje na ndani, mwenendo wa Watanzania kuhamanikia Kiingereza kama wanavyofanya sasa, utapungua. Watakapoupunguza mwenendo huo wa kuhamanikia Kiingereza ingawa hawakijui, Watanzania hao watakuwa wamepiga hatua kubwa katika ujenzi wa heba yao na utambulisho wao. Hivi sasa, Watanzania wengi waliopata ‘elimu’ wana heba ya ukimbizi katika hima yao ya kuukana Uafrika. Tatu, Mabadiliko haya yatakipa Kiswahili hadhi ya juu katika anga za biashara, na siasa ndani ya maisha ya jamii.

Uamuzi wa kukikumbatia Kiswahili nchini ni tangazo la wazi kuwa Tanzania ni Jamhuri ya Kiswahili. Tangazo hili litaandamana na kuongezeka kwa ajira kutakotokana na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili nchini. Wawekezaji – kama hiyo ndiyo hekima yetu ya leo – watumia lugha hii kwa kuendeshea biashara zao. Maana, wawekezaji hawaji Tanzania kwa sababu ni nchi ya wazungumzao Kiingereza. Wawekezaji huja kuvuna. Wafanya biashara huleta bidhaa zao. Wanapolikuta soko linazungumza Kiswahili, wao nao hawatakuwa na budi kutumia Kiswahili. Kwa misingi hiyo Watanzania watapanukiwa na ajira. Mashirika ya kigeni yatahitaji kutumia Kiswahili kwa ajili ya shughuli zao nchini. Kitakapotumika Kiswahilin na Mswahili naye atakuwapo! Tujipe nafasi ya kuangalia mchango wa wataalam.

4.2 Mchango wa Wataalamu

Kwa muda mrefu sasa – haieleweki kama ni kwa nia ya kuchelewesha utekelezaji – maagizo yanayotolewa na serkali husisitiza kazi ya kuandaa msamiati na vitabu kabla ya kuleta badiliko la sera. Lakini, kama tulivyokwishasema huko nyuma, lugha haikuzwi hivyo! Msamiati unaotakiwa katika taaluma fulani huibuka ndani ya taaluma yenyewe na wagunduzi wake ni wale wale wanataaluma wenyewe. Hivyo basi, zaidi ya kupokea istilahi za Kiingereza, mchango wa wataalamu wa fani mbalimbali ni ‘kubatiza’ viumbile (objects) wanavyokutana navyo katika taaluma hizo. Wataalam hao ndio watakaojengea lugha ya Kiswahili unyumbufu unaolingana na fani zao.

Utekelezaji wa sera mpya utakuwa changamoto kwa wataalamu wa fani hizo mbalimbali kwa sababu mbili kubwa. Kwanza sera mpya itafungua milango ya soko la vitabu vya aina mbili. Matumizi ya Kiswahili katika elimu ya juu yatazua haja ya kuwa na vitabu vya kitaalam ambavyo vimeandikwa kwa Kiswahili. Katika utekelezaji huo, vitabu vya kiada na vya ziada vitahitajika. Hivi ni kusema, sera itahimiza mchango wa wataalam wetu katika uandishi. Hali ilivyo sasa hivi, ni kwamba wasomi wetu hutegemea sana vitabu vya nje. Ni dhahiri kuwa sera hii mpya itatoa nafasi nzuri ya kuvirithisha vizazi vijavyo ujuzi wao. Aidha, sera hii itawapatia wataalam wetu fursa nzuri na pana ya kufanya utafiti na kuelimisha jamii na kupunguza mwelekeo wa kuwa ‘vipaza sauti’ vya wataalam wa nje. Wasomi wetu wataandika vitabu vyao badala ya kufasiri na kufundishia vya wenzao.

Pili uandishi wa vitabu vya ziada na kiada ni mwanzo wa ujenzi wa maktaba ya taifa la Tanzania. Urithi wa wasomi wa nchi hii – waliopo na waliopita – ni muhimu ughiliwe katika lugha ambayo kila Mtanzania anaimudu. Tena, basi, utaratibu huu, utaondoa akilini mwa kila mmoja wetu, haja ya kufikiria kufasiri vitabu vya watu wengine kwanza kabla ya

kubadilisha lugha ya kufundishia. Uandishi wa vitabu vyao wenyewe hautalijengea taifa heshima tu, bali pia utakuwa tangazo la wazi la umaizi wao kuwa, maarifa hubadilika. Isitoshe, uandishi huu, utakuwa ndio ujenzi, ingawa wa pole pole, wa maktaba ya taifa, ambao hauwezi kuligharimu Taifa kwa kiwango kisichoweza kubebeka. Tuangalie kwa ufupi jinsi vyombo vya ukuzaji lugha vitakavyochangia katika badiliko la sera.

4.3. Asasi za ukuzaji wa Kiswahili

Katika utekelezaji wa sera mpya, asasi za ukuzaji wa Kiswahili zitakuwa na jukumu kubwa la uelekezi. Baraza la Kiswahili litakuwa muhimu katika kusimamia maendeleo ya matumzi fasaha ya Kiswahili. Katika hatua za mwanzo za utekelezaji, watumiaji watahitaji msaada hata wa tahijia sahihi za maneno. Vyombo vingine vya ukuzaji, utafiti na ufundishaji wa Kiswahili vitashirikiana na Baraza la Kiswahili katika masuala mbalimbali, lakini miongoni mwa hayo, matatu yafuatayo yanahusika: mitalaa, usanifishaji na semina. Tuangalie moja moja.

4.3.1. Mitalaa

Utekelezaji wa sera hii unaandamana na mabadiliko ya taratibu za ufundishaji wa lugha nchini. Mpaka hivi sasa, mitalaa yetu haimpi mwanafunzi ujuzi wa kimawasiliano. Walimu wa Kiingereza, kwa mfano, huelekea kufundisha sarufi kuliko lugha. Badala ya kufundisha lugha walimu wamepewa kufundisha ‘uhandisi wa lugha’. Maswali ambayo wanafunzi hubebeshwa wanapokuwa ndani ya madarasa ya lugha ni kama: Kivumishi (adjective) au nomino (noun) au kiwakilishi (pronoun) ni nini? Haya ni maswali ambayo wanaisimu huulizana. Wazungumzaji wazawa wa lugha yoyote hawajui na wala hawahitaji kujua jibu la swali kama hili ili waweze kuitumia lugha yao katika mawasiliano. Sera mpya itatoa fursa ya kuweka malengo mapya ya kukifundisha Kiingereza nchini. Malengo yake yawe ya kumjengea mwanafunzi stadi za kusoma matini zake na kuzielewa. Malengo haya mapya yatalazimisha utayarishaji wa mitalaa mipya.

Katika Kiswahili pia kuna mizozo mingi sana ya kiisimu ambayo, kwa maoni yangu, haihitajiki. Kiswahili hufundishwa kama hesabu. Kwa mitalaa wa sasa, Kiswahili ni taaluma. Lakini si lazima ujuzi wa uchambuzi wa sentensi uzae ujuzi wa kukitumia Kiswahili kwa usahihi. Utekelezaji wa sera mpya unahitaji mitalaa inayojenga stadi za kusoma, kuelewa na kueleza. Mitalaa huo hauna budi kuwa na stadi zote zinazojenga umilisi kamili. Kwa kuwa stadi hizo hazawezi kupatikana katika mitalaa iliyopo, hapana budi asasi zishirikiane na wizara zinazohusika kutayarisha mipya kwa ajili ya kufundishia Kiingereza na Kiswahili kwa kulingana na malengo ya matumizi ya lugha zenyewe..

4.3.2. Semina

Asasi za ukuzaji wa Kiswahili zitahitajika kuandaa semina kwa makusudi na kwa walengwa mbalimbali. Moja ya semina hizo ni ya walimu watakaofundisha kwa Kiswahili. Semina hizi zinaweza kufanyika kwa awamu na kwa kanda. Makusudi ya semina za aina hiyo yanaweza kuwapatia misingi ya jumla kuhusu lugha ya Kiswahili na jinsi inavyopokea maneno ya kigeni. Hali kadhalika, semina za namna hii zitasaidia kuanzisha mawasiliano ya kudumu kati ya shule na asasi hizo. Mawasiliano hayo yatakuwa na manufaa katika uwekaji wa kumbukumbu za ubunifu wa walimu katika upanukaji wa msamiati wa kitaalam.

Aina nyingine ya semina inaweza kuwa ya uelimishaji kuhusu matumizi ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali za maisha ya taifa. Semina ya aina hii itawasaidia Watanzania wajenge aina ya ‘woga’ utakaowawezesha kukitumia Kiswahili kwa kuendelezea mahusiano yanayokusudiwa. Mfanyabiashara anayemwambia mteja wake ‘*changamka!*’ ‘*Bi mdogo*’. ‘*Babu!*’ n.k. hana habari kuwa matumizi ya maneno hayo huweza kuleta karaha kwa mteja. Asasi za Kiswahili, kwa ubunifu wao, wataweza kuchanganua ulimwengu wa Kiswahili na kuona maeneo mbalimbali ya matumizi yanayohitaji kuelimishana.

4.3.3. Usanifishaji

Mwisho, Baraza la Kiswahili kwa kushirikiana na asasi za ukuzaji na utafiti wa lugha, lina wajibu wa kusanifisha istilahi zinazozaliwa wakati sera inapotekelezwa. Kwa vyovyote vile, zitazuka istilahi nyingi kwa dhana moja. Kazi ya vyombo vya ukuzaji itakuwa kuteua moja au mbili na kuacha nyingine. Hali kadhalika, kwa kuwa msamiati wa Kiswahili, kwa sehemu kubwa, umo mwenye makamusi tu, vyombo vya Kiswahili vitatoa mchango wa kuibua maneno ya Kiswahili ambayo yana uwezo wa kuchanua dhana zinazohusika. Mfano mzuri ni wa neno la Kiingereza ‘*Arrears*’. Watu wengi hawajui kabisa kuwa Kiswahili kina neno ‘*karisaji*’ kwa maana hiyo hiyo. Aidha, watu wengi hawajui kuwa *elevator/lift* hufasirika kwa neno la Kiswahili *kambarau*. Kwa mantiki hiyo, vyombo vya Kiswahili vina wajibu wa kudhihirisha uwezo wa kimsamiati ambao Kiswahili tayari kinao.

Usanifishaji ni fursa nzuri ya kuzipatia lugha za kikabila nafasi nzuri ya kutoa mchango katika kujaza mapengo yaliyopo ya msamiati. Kama Kizigua kwa mfano, kina neno moja *nguju* kwa maana ya maneno matatu ya Kiswahili ‘*mbegu za maboga*’, au *safe* kwa maneno mengine matatu ya Kiswahili *majani ya kunde* sioni mhali kama neno ‘*nguju*’ au *safe* litachukuliwa badala ya *mbegu za maboga* au *majani ya kunde*.

Katika hima hiyo hiyo, vyombo vya ukuzaji lugha vina wajibu wa kutengeneza kamusi kubwa ambalo litaorodhesha maneno yote au karibu yote ya Kiswahili. Kamusi hilo lisitayarishwe kwa misingi ya biashara, bali litayarishwe nakala chache kwa ajili ya matumizi ya rejea. Kamusi la aina hii litasaidia sana katika matayarisho ya ujenzi wa ufasiriano wa Kiingereza na Kiswahili katika hatua ya kwanza. Maana kwa kuwa Kiingereza kitaendelea kutumika, baada ya kuwa na kamusi hilo kubwa, ndipo jitihadi zitafanyika kutayarisha makamusi mawili: Kiingereza-Kiswahili na la Kiswahili-Kiingereza. Utekelezaji wa sera hii mpya utategemea kiwili kamili kati ya viongozi wa serkali, wataalam wa fani zote pamoja na wananchi kwa ujumla.

5. Mwisho

Utekelezaji wa sera mpya, kwa sehemu kubwa, huandamana na mambo, takriban, mane. Kwanza unahitajika uchambuzi wa tatizo. Uchambuzi huo ndio unaotuwezesha kutoa tamko la sera. Tamko la sera ambalo ni la serkali hupanga majukumu ya lugha zilizomo ndani ya jamii. Wanajamii, kila mmoja kwa nafasi yake, hutoa mchango wake kwa kuzitumia lugha zinazohusika kwa mujibu wa tamko. Papo hapo, kwa kuzitumia lugha hizo wanajamii hao, kila mmoja kwa nafasi yake, hujenga umilisi wa lugha hizo kulingana na fani yake. Isitoshe, matumizi ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali hukipatia fursa ya kujijengea unyumbufu.

Mchango wa vyombo vya ukuzaji ni ule wa kuratibu kuelekeza na kuweka kumbukumbu. Hali kadhalika, kwa kuwa wao ndio wataalam wa isimu, watakuwa karibu zaidi na watumiaji katika kuwapa ushauri wa kitaalam kuhusu utohoaji wa maneno ya Kiingereza yatakayoingia katika Kiswahili. Maneno hayo hayana budi yapate uenyeji wa kifonolojia na kimofolojia katika Kiswahili. Wakuzaji wa lugha watatakiwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kuna walimu weledi wa lugha hizi zinazofundishwa. Mitalaa yote ya lugha itakuwa ni mchango wao.

MAREJEO

- Fishman, J.A. (1971) in Whiteley, W.H. (1971) *Language Use and Social Change: Problems of Multilingualism with Special Reference to Eastern Africa*. Oxford University Press for International African Institute.
- Hammerly, H. (1982) *Synthesis in Second Language Teaching: An Introduction to Linguistics*. Blaine, W.A. and Second Language Publications.
- Heugh, K. (1999) 'Languages, Development and Reconstructing Education in South Africa' in *International Journal of Educational Development* (Special Issue) Vol. 19 Nos 4-5 July – September 1999. Guest Editor, Leshe J. Limage Pergamon.
- Klein, W. (1986) *Second Language Acquisition*. Cambridge University Press. Cambridge, New York, New Rochelle, Melbourne, Sydney.
- Makweta, J. (1982) *Mfumo wa Elimu ya Tanzania 1981 – 2000: Ripoti na Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Elimu*. Juzuu la Kwanza. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dar es Salaam.
- Maxwell, Kevin, B. (1983) *Bemba Myth and Ritual: The Impact of Literacy on an Oral Culture*. Peter Lang Publishing Inc. New York. Frankfurt on The Main, Berne.
- Mazrui, A. (1997) 'The World Bank: The Language Question and the Future of African Education' in Heugh (op.cit)
- Mochiwa, Z.S.M. (1991) 'Bifocalism or Umforcalism in Education? A Critical Evaluation of Language Policy in Tanzania' in *Issues in Language and Education* (ILE) #4. Boston. African Studies Center. Boston University.
- (1999) 'Elimu au Maigizo? Uhakiki wa Sera ya Lugha katika Elimu Tanzania'
- (1999) 'Utoto hadi Ungumbaru: Matatizo ya Elimu Tanzania' katika Tumbo-Masabo n.w. (1999) *Kiswahili katika Elimu*. TUKI – Dar es Salaam
- (2000) 'Subtractive Multilingualism: An Educational Legacy in Tanzania?' Kuchapishwa katika *Journal of Language and Linguistics*. Foreign Language and Linguistics. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mulokozi, M.M. (2000) Language Literature and the Forging of a Pan-African identity – ilitayarishwa kwa ajili ya mkutano wa kimataifa ulioitwa: "Africa: Society, Culture and Languages: Man in Socio-Cultural Space". St. Petersburg, Russia 16-18 May, 2000.
- Nyerere, J.K. (1967) *Education for Self-Reliance*. Government Printer. Dar es Salaam.
- Pool, J. (1972) 'National Development and Language Diversity' in Fishman, J.A. (ed) *Advances in the Sociology of Language II*